

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Anwani ya Simu: “**Mifugo**”
Simu Nambari: +255 (026) 2322612
Nukushi: +255 (026) 2322613
Barua pepe: ps@mifugo.go.tz
Tovuti: <http://www.mifugouvuvi.go.tz>



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2870,
DODOMA

**TANGAZO LA VIJANA KUJIUNGA NA VITUO VYA JENGA KESHO ILIYO BORA
(BBT) VYA UNENEPESHAJI WA NG'OMBE WA NYAMA KIBIASHARA**

1. Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakaribisha maombi ya Vijana kujiunga na mafunzo ya Ujasiriamali kupitia Programu ya BBT – Mifugo ya unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama kibiashara kwa muda usiozidi mwaka mmoja katika vituo vifuatavyo:-

NA	KITUO	MKOA	IDADI YA VIJANA
1	LITA Buhuri	TANGA	60
2	LITA Mabuki	MWANZA	60
3	LITA Kikulula	KAGERA	60
4	TALIRI Tanga	TANGA	30
5	TALIRI Mabuki	MWANZA	30

2. Waombaji watatoka katika makundi matatu kama ifuatavyo:-
- i. Asilimia 30 ya vijana wawe ni wahitimu wa angalau elimu ya msingi wanaojishughulisha na ufugaji wa ng'ombe.
 - ii. Asilimia 30 ya vijana wawe wamehitimu mafunzo ya kujitolea ya Jeshi la Kujenga Taifa.
 - iii. Asilimia 40 ya Vijana wawe wamehitimu Mafunzo ya Mifugo katika ngazi za Astashahada, Stashahada au Shahada kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali.
3. Sifa za muombaji
- i. Awe Raia wa Tanzania,
 - ii. Awe na umri kati ya Miaka 18 – 30,

- iii. Awe ni Kijana mwenye tabia njema na barua yake ya maombi ipitishwe na uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa anapoishi,
- iv. Awe tayari kushiriki mafunzo kwa vitendo katika shughuli za ufugaji mifugo kibiashara katika kipindi husika,
- v. Awe tayari kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa katika kituo atakachokuwa akifanyia shughuli za ufugaji kibiashara, na
- vi. Awe mwenye afya njema itakayomwezesha kushiriki mafunzo kikamilifu. Muombaji aambatishe cheti cha uthibitisho wa daktari kutoka katika hospitali inayotambulika na Serikali.

4. Fomu ya kujiunga na vituo hivi inapatikana kupitia tovuti za Wizara ya Mifugo na Uvuvi (www.mifugouvuvu.go.tz) au Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (www.lita.go.tz) au Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (www.taliri.go.tz). Fomu za maombi kwa wahitimu wa vyuo vya Mifugo na Jeshi la Kujenga Taifa ziambatishwe na nakala za vyeti vilivyothibitishwa. Aidha, waombaji wote wawasilishe nakala za vitambulisho vya NIDA vya mwombaji na nakala ya kitambulisho cha mdhamini.

5. Fomu hiyo ya maombi na viambatisho vitumwe kupitia barua pepe barua@lita.go.tz au hq@taliri.go.tz


6. Waombaji watakoachaguliwa katika hatua ya kwanza wataitwa kwa ajili ya usaili kwa vitendo katika vituo walivyochaguliwa. Waombaji wawe tayari kujigharamia nauli, chakula na malazi wakati wa usaili kwa vitendo vituoni.

7. Mwisho wa kupokea maombi ni wiki tatu baada ya tangazo kutoka.

Kwa ufafanuzi zaidi, Wasiliana na:-

	Taasisi	Mawasiliano -Simu
1	Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA):	0625 874 298 au 0742 762 364
2	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI):	0763 546 165 au 0785 325 847

Imetolewa na;



Prof. Riziki S. Shemdoe
KATIBU MKUU
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI